Kijana Tajiri
(The Rich Young Ruler)

na

Ellis P. Forsman

Kijana Tajiri
(The Rich Young Ruler)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kijana Tajiri

Mat. 19:16-22

Mat. 19:16-22, "*Na tazama mtu mmoja akamwendea, akamwambia mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia kwa nini kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja tu. Lakini ukitaka kuingia katika uzima zishike amri. Akamwambia zipi? Yesu akasema ni hizi, usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba yako na mama yako, na mpende jirani yako kama nafis yako. Yule kijana akamwambia haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena? Yesu akamwambia ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*"

Hadithi ya kijana huyu ni moja inayovutia sana, na bado ni moja ya ghadhabu inayoweza kupatikana katika Agano Jipya.

Anakuja kwa Yesu kwa matarajio alafu anaondoka kwa huzuni.

Hadithi hii inayokatisha tamaa ni moja inayopatikana katika Agano Jipya.

Hakuna hadithi ambayo mtume wa Yesu aliwahi kuanzisha iliyo na taraja kama hii. Wakati mmoja tunamwona anamwendea Yesu; na wakati mwingine anatoweka, akishikilia maliza zake kwa moyo uliovunjika.

Tuangalie mambo matatu kuhusu hadithi hii:

- Kijana huyu alikuwa nani.
- Swali lake la taraja.
- Majibu ya Yesu.
- Kuondoka kwake kwa huzuni.

Kijana huyu alikuwa nani

Katika mtazamo wa kidunia.

Alikuwa kijana.

Mat. 19:20, "*<u>Yule kijana</u> akamwambia hata yote nimeyashika nimepungukiwa na nini tena?*"

Ujana ni kitu ambacho dunia hii iliyozeeka inaipa thamani ya hali ya juu. Huyu kijana alimiliki ujana; alisimama katika asubuhi ya maisha.

Huu ni wakati mwafaka katika maisha kwa mtu kujitoa kwa ajili ya Kristo; kabla ya tabia mbaya hazijaingia.

Nyak. 12:1, "*Mkumbuke muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema, mimi sina furaha katika hiyo.*"

Timotheo alianza katika ujana akifanya kazi na mtume Paulo.

1 Tim. 4:12, "*Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo na katika upendo na imani na usafi.*"

Alikuwa mtawala.

Luka 18:18, "Tena mtu mkubwa mmoja alimwuliza, aakisema mwalimu mwema nifanye nini ili niweze kuurithi uzima wa milele?"

Alikuwa na sehemu, wadhifa, na uwezo; vilevile alikuwa mtu anayeshawishi.

Alikuwa na mali.

- Mat. 19:22, "*Yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*"
- Luka 18:23, "*Lakini aliposikia hayo alihuzunika sana, maana alikuwa na mali nyingi.*"

Inakwenda bila swali kwamba dunia hii iliyozeeka inazingatia mali kama kitu chenye thamani. Pesa ina nguvu; pesa inaongea.

Hataivyo, hakuwa tajiri mbele ya Mungu.

Luka 12:21, "*Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.*"

Toka katika msimamo wa kimbingu.

Alikuwa mtu mwema. Alikuja akikimbia kwa Yesu.

Marko 10:17, "*Hata alipotoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?*"

Alikuja na shauku kubwa kwa Yesu.

Alikuwa mnyenyekevu. Alipiga magoti mbele ya Yesu (angalia msitari hapo juu). Alikuja kwa roho ya ukarimu; hakuwa na sifa mbaya.

Katika kupiga magoti, alimtambua Yesu kama wa kipekee na akamwabudu.

Wengine walimwendea Yesu ili miili yao iponywe, lakini hapa kuna moja inayoidai roho yake.

Alikuwa mwenye heshima.

Anamwongelea Yesu kama "Mwalimu".

Mat. 19:16, "*Na tazama mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele?*"

"Mwalimu" lilikuwa ni jina ambalo Wayahudi walikuwa na tabia ya kulitumia kwa waalimu wao wa kidini.

Hivyo, alikuja katika roho ya mwanafunzi kujifunza hekima kutoka kwa "Mwalimu mwema."

Alikuwa mtu anayeheshimiwa.

Mat. 19:20, "*Yule kijana akamwambia haya yote nimeyashika, nimepungukiwa na nini tena?*

Kwa vile alikuwa mtu mwenye taarifa nzuri.

"*Nimepungukiwa na nini?*"

Kama ukimhukumu kwa dunia, alikuwa na ujana, mvuto, na tajiri.

Kama ukimwangalia kwa mtazamo wa kimbingu, alikuwa na shauku, mkarimu, mwenye nidhamu, na mwenye heshima.

Kwa vile angeweza kusimama juu katika dunia na awe na nidhamu nzuri katika mtazamo wa kimbingu.

Watu wengi wangesema kwamba anafaa kwa ajili ya mbingu.

Lakini uadilifu pekee hautoshi katika macho ya Mungu.

- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia, na kweli na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"
- Mdo. 4:12, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"
- Rum. 6:17, "*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*"

Wapo watu wengi wema, watu waadilifu katika dunia ambao bado hawajamtii Kristo; hawajatii elimu ya wokovu aliouanzisha.

Swali la kutarajiwa la kijana (hakika maswali mawili)

Mat. 19:16, "*Na tazama mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele?*"

Bila shaka alifundishwa na waalimu wa Kiyahudi kwamba watu wanaokolewa kwa kutenda jambo.

- Mika 6:6-7, "*nimkaribie BWANA na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliyejuu? Je! Nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? Je! BWANA atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambia ya roho yangu?*"
- Mat. 19:20, "*Yule kijana akamwambia haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena?*"

Lakini kitu kimoja kinaweza kumanisha kila kitu. Kama ufunguo katika gari; spiringi kwenye saa; au rada kwenye meli.

Hakukoswa ujana, mvuto, utajiri, ukarimu, kutokuheshimiwa, au kutojituma.

Lakini alikoswa uzima wa milele – uzima huo unatoka kwa Mungu anayejua pekee kupitia Yesu Kristo.

Yoh. 17:3, "*Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo aliyemtuma.*"

Jibu la Yesu lenye kushtusha (hitaji upande kuwili).

Mat. 19:21, "*Yesu akamwambia ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate.*"

"*Ukitaka kuwa mkamilifu*" ("Kamili").

"Kama ukigawa kile kinachopungua na ufanye utii wako ukamilike."

"*Enenda ukauze ulivyo navyo*" (weka vilivyo vyako wakfu kwa Mungu).

Kwa nini? Yesu aliona kwamba amefanya utajiri wake mapambo. Yesu alimtaka aondoe pambo katika moyo wake.

"*Kisha njoo unifuate.*"

Hii ilikuwa ni lazima. Yesu hakuwa kwa ajili ya kuuza na kugawa.

Alikuwa kwa ajili ya kijana kumfuata na kumsaidia, kama jinsi alivyowaomba mitume wengine.

Mat. 4:19-22, "*Akawaambia nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Mara wakaziacha nyavu zao wakamfuata. Akaendelea mbele akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwamo chomboni pamoja na Zebedayo Baba yao, wakizitengeneza nyavu zao; akawaita.mara wakakiacha chombo na baba yao wakamfuata.*"

Kuondoka kwa kijana kwa huzuni

Mat. 19:22, "*Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*"

Ni jinsi gani alivyokuja kwa Yesu.

Yeye aliyekuja "*akikimbia na kupiga magoti*" kwa taraja ya hali ya juu, sasa anatembea taratibu akiwa na huzuni.

Hivyo, alishindwa kuwa mwanafunzi wa Kristo

Lakini kwa nini aliondoka?

Siyo kwa sababu Yesu hakuwa mkarimu kwake.

Marko 10:22, "*Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*"

Lakini kwa sababu "*alikuwa na mali nyingi*".

Alijaribu kushikilia hazina zote za dunia mbili.

Mat. 6:24, "*Hakuna awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*"

Mat. 16:26, "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*"

Udanganyifu wa mali ulifuta neno la Yesu katika roho yake, na hivyo kuutia upofu hukumu yake ambayo asingeweza kuitii.

Hitimisho

Kumbuka neno la Yesu kwa mitume wake mara ikifuatiwa na tukio hili:

Mat. 19:23-24, "*Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amini, nawaambieni ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa*

mbinguni. Nawaambia tena ni rahisi ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."

Alafu mitume walisema "*ni nani basi awezaye kuokoka?*" (Mat. 19:25).

Hakuna awezaye kuokolewa anayekataa kutimiza misingi ya wokovu.

Yeyote anayependa, anaweza kuokolewa.

Ufu. 22:17, "*Na Roho na Bibi arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo! Naye mwenye kiu na aje; nay eye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.*"

Kama ukiuliza, kama alivyofanya huyu kijana, "*Nifanye… ili niwe na uzima wa milele?*"

Leo, Bwana anakuagiza ku:

Kumwamini Bwana Yesu Kristo. Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Tubu dhambi zako.

- Luka 13:3, "*Nawaambia sivyo; lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.*"
- Mdo. 17:30, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*"

Kiri jina la Yesu.

- Mat. 10:30, "*Lakini ninyi hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote.*"
- Mdo. 8:37, "*Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu, akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.*"
- Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinya chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Ubatizwe kwa ajili ya ondole la dhambi.

- Mat. 28:19, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;*"

- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"

Sasa unaonana na Kristo yule yule ambaye huyu kijana tajiri alikutana naye.

Alikuwa na nafasi yake lakini akaitupa; bado unayo yako.

Kristo aliyempigania, sasa anakupigania.

Kristo aliyemkaribisha amtumikie, sasa anakukaribisha.

Jibu <u>lako</u> litakuwa nini?